Toleo 50

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## WANAWALI KUMI

(Mathayo 25:1-13)

Yesu alifundisha somo kuu la mfano wa wanawali kumi, na akatumia mfano huo kufundisha haja ya sisi kuwa tayari kwa mambo ya kiroho. Mfano huu unatufanya tujichunguze kindani. Kuja kwa pili kwa Yesu kunafananishwa na sherehe ya arusi, ambapo Yesu, Yeye ambaye ndiye bwara-arusi anarudi ili kumpokea bibi-arusi wake, ambaye ndiye kanisa. Mfano huu unatuhimiza kwamba tuwe macho, na pia unatuonya kuhusu umuhimu wa kujiandaa kwa ajili ya kurudi kwake Yesu.

Wanawali kumi, kila mmoja wao akiwa amebeba taa, waliondoka ili kumlaki bwana-arusi. Watano wao wanaelezwa kwamba walikuwa wenye hekima, ilhali wale wengine wanaelezwa kwamba walikuwa wapumbavu. Tofuati kuu kati ya vikundi hivi viwili vya wanawali ilikuwa katika hali yao ya maandalizi;: wale watano wenye hekima walibeba mafuta ya ziada kwa ajili ya taa zao, ilhali wale wapumbavu hawakufanya hivyo. Walipokuwa wakimsubiri bwana-arusi, ambaye alikuwa amekawia, wanawali wote walichoka na usingizi ukawapata. Lakini usiku wa manane ukelele ukasikika: "Haya, bwana arusi ndiye huyu; tokeni mwende mkamlaki."

Walipoamka, wanawali hao walichana taa zao kuhakikisha kwamba zingewaka vizuri. Ndipo wale wanawali wapumbavu wakatambua kwamba taa zao zilikuwa zimezima mwanga kutokana na upungufu wa mafuta. Huku wakiwa na mshtuko mkubwa, waliwaomba wanawali wenye hekima wawagawie mafuta yao. Lakini wanawali wenye hekima walikuwa na mafuta yaliyotosha tu kwa ajili ya mahitaji yao wenyewe, ndiposa wakawapatia mawaidha wanawali wapumbavu kwamba waende wajinunulie mafuta yao wenyewe.

Wakati wanawali wapumbavu walikuwa wangali safarini ya kununua mafuta, bwana-arusi akafika. Wale ambao walikuwa wamejiandaa—wenye hikima—wakaingia kwenye sherehe ya harusi pamoja na bwana-arusi, na mlango ukafungwa. Na wakati wanawali wapumbavu waliporudi, waliomba kwamba wafunguliwe mlango huku wakisema, "Bwana, Bwana, utufungulie." Lakini bwana-arusi akawajibu akawaambia, "Amin, nawaambia, siwajui ninyi."

Yesu alitamatisha mfano wake kwa kutoa onyo kali: "Basi kesheni, kwa sababu hamwijui siku wala saa mwana wa adamu atakaporudi." Onyo hili linatilia mkazo umuhimu wa sisi kudumu katika hali ya utayari wa kurudi kwake Kristo.

Ili kutoa tafsiri ambayo inafaa kwa swala kuu ambalo linafundishwa kwenye mfano huu, ni muhimu sisi kutambua kwamba sio maelezo yote yaliyo kwenye hadithi ya mfano huo yanatakiwa kuwa na maana fulani (ya mafundisho) ya kidini. Maana ya mfano ni hadithi ambayo ilikuwa inafundisha ukweli mmoja mkuu, na kuongezewa maelezo mengine ili kuwasaidia wasomaji kuweza kuelewa mfano wenyewe, bali maelezo hayo hayaashiri kwamba kuna ukweli mwingine maalum ndani yake. Na katika mfano huu, wanawali kumi hawawakilishi watu ambao hawajaamini, bali wanawakilisha Wakristo binafsi ambao wanadai kwamba wao wako safi kwa maswala ya maadili, kwamba hawajapakwa uchafu na ulimwengu, na ambao pia ni wafuasi wake Mungu.



Lakini usiku wa manane ukelele ukasikika: "Haya, bwana arusi ndiye huyu; tokeni mwende mkamlaki."

Mgawanyiko uliokuwako kati ya wanawali wenye hekima na wale wapumbavu haumaanishi kwamba ni asilimia hamsini pekee ya wale wanaojiita Wakristo ndio wataokoka; bali huu ni wito wa kuwaambia Wakristo wazinduke, ili kutathimini hali yao ya kiroho. Wakati wanawali wote walipokuwa wakimngojea bwana-arusi, ni wale tu waliokuwa na hekima ndio walikuwa tayari kwa ajili ya kufika kwake bwana-arusi.

Jinsi bwana-arusi alivyochelewa ndivyo wanawali hao wote walivyochoka, wakasinzia, na kuanza

*(Endelea katika Ukurasa 2)*


| Tahariri | Mwongozo wa Kujifunza Biblia: Matendo ya Haki | Mavazi ya Haki | Maswali na Majibu | Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| 3 | 4 | 5-6 | 7 | 8 |

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)*
kupatwa na usingizi. Jambo hili linafananishwa na uchovu wa kiroho na mwelekeo wa kuchukulia mambo hivi hivi ambalo ni jambo linalowaingia Wakristo wanapokuwa wakisubiri kurudi kwake Kristo. Ulimwengu huu umejaa shida na mambo mengine yanayotupeleka mbali na Kristo, na pia majaribu. Ndiposa kuchelewa kwa kurudi kwa Kristo kunaweza leta hali ya kutojali kwa swala la sisi kudumisha utayari wetu wa kiroho. Wale wanawali wapumbavu ambao walimtarajia bwana-arusi kufika mapema hawakujiandaa vya kutosha, na ndiposa wakapuuza swala la kubeba mafuta tosha kwa ajili ya taa zao. Mafuta hayo yanaashiria uwepo wa Roho Mtakatifu maishani mwetu kama waumini wa Kristo.

Lakini wale wanawali waliokuwa na hekima walikuwa wamejiandaa vizuri na kubeba mafuta tosha ya kuwezesha taa zao kuendelea kuwaka. Kulikuwa na uhusiano ulio hai na wa kweli kati yao na Mungu, uhusiano ambao ulidumishwa kwa nguvu zake Roho Mtakatifu. Imani yao haikuwa tu katika matendo ya kuonekana, ya kusema kwamba wao ni watu wazuri, bali kiini cha imani hiyo kilikuwa katika nguvu za Roho Mtakatifu zinazomdumisha mtu, jambo ambalo liliwawezesha kuendelea kung'aa katika ulimwengu uliojaa giza.

Bwana-arusi alipofika wanawali wenye hekima walikuwa tayari na walikaribishwa katika sherehe ya arusi. Sherehe hii ya arusi inawakilisha upatanisho wa mwisho kati ya Kristo na Kanisa lake, wakati ule ambapo muda utafika kikomo. Na wakati mlango ulipofungwa, hakukuwa na nafasi nyingine ya wanawali wapumbavu kuingia. Jambo hili linawakilisha hukumu ya mwisho ambayo itatolewa wakati Kristo atakaporudi. Wakati huo hakutakuwa na muda wa ziada wa kuomba, wa kutafuta uvuvio wa kiroho, wa kutakaswa, au wa kupewa nguvu mpya na Roho Mtakatifu. Hakutakuwa na nafasi ya ziada.

Moja ya mambo mazito katika mfano huu ni vile ambavyo bwana-arusi aliwajibu wanawali wapumbavu: "Amin, nawaambia, siwajui ninyi." Jambo hili linadhihirisha hatari ya sisi kutegemea matendo ya kiinje au ya kuonekana ya imani, bila kuwa na hali ya kiroho ambayo ina kina ndani mwetu. Hata ingawa wanawali wapumbavu walionekana kuwa wanamsubiri bwana-arusi, hawakuwa tayari, na pia walikuwa na ukosefu wa hali halisi ya uhusiano wa kweli kati yao na Mungu. Walikuwa na sifa za uungu wa kuonekana kwa nje, lakini ndani yao walikosa moto wa kweli wa Roho wa Mungu.

Kila muumini anahitaji kujichunguza utayari wake wa kiroho. Je, wewe umo kati ya wenye hekima au wapumbavu? Je, una mafuta ya Roho Mtakatifu maishani mwake, au unategemea matendo na mazoea ya nje ya vitendo vya kidini? Basi wewe mtu ambaye hauna umakini, hebu zinduka na utoke kaika hali hiyo ya kusinzia kwako kwa kiroho, ili ujiandae kwa ajili ya kurudi kwake Bwana.

Ujumbe huu uko wazi; ni kwamba tuwe macho na tuwe tayari kwa sababu hakuna hata mmoja wetu tunayejua Kristo atarudi lini. Huu ndio wakati ufaao wa kujiandaa. Ikiwa ndani yako hakuna moto unaowaka wa Roho Mtakatifu maishani mwako, hebu basi usichelewe tena. Mweke wako uko wazi sasa, lakini hautadumu katika hali hiyo milele. Tarumbeta ya mwisho itakaposikika ndipo hapo mlango utakapofungwa.

Je, wewe uko tayari kukutana na bwana-arusi? Sasa ndio wakati ambao unafaa! ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



*Haki huinua taifa; bali dhambi ni aibu ya watu wo wote.* —Mithali 14:34

Andiko hili kutoka Kitabu cha Mithali lina ukweli mkubwa ambao ni zaidi ya maana yake ya kithiolojia katika lugha ya asili ya Kiebrania. Kijuujuu, tunaweza kusema kwamba Mungu huwa kwenye upande wa mataifa na watu ambao hukubali haki na kuishi maisha yenye maadili bora na pia kwamba Yeye huyabariki. Kwa upande mwingine dhambi ni kitu kiovu na huleta aibu na lawama kwa watu wote. Hata ingawa tunaishi katika ulimwengu ambao umejaa dhambi, na ukosefu wa haki ni jambo ambalo limesambaa kote, tunaweza kupata tumaini katika neema ya kiungu ambayo ina nguvu zaidi kushinda nguvu za dhambi.

Somo la robo hii ya mwaka ni, "Mavazi ya Haki." Wakati mmoja huku nikiwa kazini ya umisheni nilipata maono na ujumbe uliohusiana na "Bibi-arusi wa Kristo." Maono hayo yaliniongezea uelewaji wangu wa Kanisa kama bibibi-arusi wa Kristo, na kunipa mwanga zaidi kuhusiana na swala la urembo wa kanisa, na pia usafi wake. Ombi langu ni kwamba, mafunzo yaliyo hapa yatamguza kila msomi na kumwelekeza kwa uelewaji zaidi wa haki ya kweli. Hebu basi Roho Mtakatifu afanye kile ambacho maneno matupu hayawezi kufanya.

*Tutembelee www.thegospeltruth.org ili kujiandikisha na kupata jarida za mbele.*

Kanisa, ambalo ni mfano wa bibibi-arusi, limeitwa na Mungu ili liwe safi, takatifu, lenye uungu, na ambalo liko tayari kwa ajili ya kurudi kwake Bwana. Na kweli kanisa sio dhana ambayo haieleweki vizuri, bali ni mwili wa waumini. Basi kila muumini anahitaji kuvalishwa haki yake Mungu. Na hata ingawa kuna mijadala mingi kuhusiana na maana ya dhambi, na pia kuhusu tabia za kilimwengu ni zipi; na zaidi ya hayo kuna lawama ambazo zimetolewa kuhusiana na viwango vinavyofaa vya Kanisa kwa swala la utakatifu. Swali ni, je, ni kwa nini hatuwezi kutulia kidogo na kufanya juhudi za kupata maono ya kiungu ya bibi-arusi wa Kristo? Hebu basi tuweke kando kwa muda mawazo yetu, misimamo yetu, dhana zetu za mbeleni, na tamaduni zetu za kawaida ili tuweze kufungua mioyo yetu na akili zetu kwa Neno lake Mungu na Roho wake Mtakatifu, huku tukitafuta ufunuo mkuu zaidi kwa swala hili la haki.

Je, Mungu ana shauku ya kufanya nini mioyoni mwetu na maishani mwetu? Ikiwa tumeokoka, sisi ni sehemu ya kanisa lake. Kulingana na ukweli huu tunahitaji kuishi vipi na kutenda vipi? Migogoro hufika kikomo wakati tunapotazama mambo kwa miali ya haki ya Mungu. Kama bibi-arusi wa Kristo, lengo letu linastahili kuwa ni kumpendeza Mungu na kuepukana na matendo na athari ambazo zimejaa tamaa za mwili, tamaa za macho, na kiburi cha maisha.

Tukitazama urembo unaoletwa na haki, tunapata hali nzito na changamoto ya sisi kuyachunguza maisha yetu na kuhakikisha kwamba yanaambatana na utakatifu wake Mungu. Sisi sote tumekosa ukamilifu, lakini lengo letu linastahili kuwa ni kufanya maisha yetu yafanane zaidi na Kristo, huku tukimruhusu Roho Mtakatifu kutuunda na kutukarabati. Kwa jinsi ambavyo uchafu kidogo unaweza kuharibu maji yote yaliyoko kwenye kikombe, ukosefu mdogo wa haki unaweza kuleta athari katika roho zetu.

Hebu basi tutazame usafi wa bibi-arusi, na tufanye bidii kutafuta maisha ya haki na kuishi kwa njia ambayo imekubalika na Mungu.

Michael W. Smith

Oktoba, 2024

## Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu?

(1 Wakorintho 6:9-10)

Waasherati

| | | | |
|---|---|---|---|
| Waabudu sanamu | Wazinzi | Wevi | Walevi |
| | Walawiti | Watamanio | Wanyang'anyi |

WADHALIMU



# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Somo: Matendo ya Haki

**Masomo ya Maandiko:** *Arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari. Naye amepewa kuvikwa kitani nzuri, ing'arayo, safi; kwa maana kitani nzuri hiyo ni matendo ya haki ya watakatifu.* —Ufunuo 19:7-8

**Maana:** Matendo ya haki "Ni kutenda kulingana na sheria ya kiungu au ya maadili bora. Ni kuwa huru kutokana na hatia ya dhambi" (*Kamusi ya Merrian-Webster*). "Mafundisho kuhusu jinsi mwanadamu anaweza kufikia hali ya kukubalika na Mungu. Sifa bora, matendo mema, usafi wa maisha, kuwa katika hali ya haki, kuwa na mawazo yanayofaa, hisia pamoja na matendo" (*Thayer*).

Muhtasari: Kanisa ni bibi-arusi ambaye anangojea kuja kwa bwana-arusi. Ndiposa kanisa linahitaji kuvalishwa mavazi meupe ya haki. Watoto wa Mungu wanastahili kuishi maisha ya haki na utauwa, huku wakiwa wamejiandaa kwa kurudi kwake Yesu Kristo.

### I. Bibi-arusi wa Kristo

A. Ufunuo 21:1-2 Kupambwa kwa ajili ya mumewe.
B. Ufunuo 21:9-11 Bibi-arusi, mke wa Mwana-kondoo.
C. Waefeso 5:25-27 Lisilo na ila wala kunyanzi.
D. 2 Wakorintho 11:2 Bikira safi.

### II. Mavazi Meupe ya Watakatifu

A. Ufunuo 19:7-9 Kitani nzuri hiyo ni matendo ya haki ya watakatifu.
B. Ufunuo 3:4-5 Wamevaa mavazi meupe.
C. Ufunuo 7:9 Watakatifu mbinguni wamevikwa mavazi meupe.

### III. Mtumikieni Bwana kwa Haki

A. Luka 1:74-75 Kumwabudu Bwana kwa haki.
B. 1 Yohana 3:6-8 Wale wakaao ndani yake Kristo hawatendi dhambi.
C. Warumi 6:18-19 Watumishi wa haki.
D. 1 Wakorintho 6:9-10 Matendo ya udhalimu.

### IV. Wito wa Kuwa Wenye Haki

A. Mathayo 6:33 Tafuteni haki yake.
B. 1 Timotheo 6:11 Fuateni haki.
C. Waefeso 4:24-25 Vaeni utu mpya.

### V. Kwa Imani Sio kwa Sheria

A. Wagalatia 2:16 Hatuhesabiwi haki kwa matendo ya sheria.
B. Warumi 5:1 Kuhesabiwa haki kwa imani.
C. Warumi 5:18-21 Sisi ni wenye haki kupitia kwa Kristo.

### VI. Haki Yetu ya Kibinafsi Haitoshi

A. Wafilipi 3:7-9 Sio haki yangu mwenyewe.
B. Warumi 10:3-4 Kuidhibitisha haki yao wenyewe.
C. Isaya 64:6 Haki yetu ni kama nguo iliyotiwa unajisi.
D. Tito 3:5 Sio kwa matendo yetu ya haki.
E. Mathayo 5:20 Haki zaidi ya Mafarisayo.
F. Mathayo 23:27-28 Kuonekana kwa nje.

### VII. Wito wa Haki

A. 1 Petro 1:18-19 Hatujakombolewa kwa vitu.
B. Wagalatia 6:15 Kutahiriwa au kutotahiriwa sio mambo muhimu.

### VIII. Asili ya Kiungu

A. 1 Wakorintho 15:34 Amkeni ili mtende mema.
B. 2 Timotheo 3:16 Maandiko yafaa kwa ajili ya kufundisha.
C. Isaya 28:17 Kanuni na timazi.
D. 1 Wakorintho 6:9-10 Wadhalimu hawataurithi.

### IX. Bibi-arusi Alinganishwa na Kahaba

A. Ufunuo 12:1 Mwanamke aliyevikwa jua.
B. Ufunuo 17:1-6 Kahaba mkuu.
C. Isaya 1:21-22 Mji mwaminifu unakuwa kahaba.

### X. Ahadi kwa Wenye Haki

A. 1 Petro 3:12 Masikio yake husikiliza maombi yao.
B. Matendo 10:35 Kukubaliwa na Mungu.
C. 1 Petro 3:14 Mna heri.
D. Mathayo 5:6 Wana heri.
E. 2 Timotheo 4:7-8 Taji la haki.

### XI. Mavazi Yasiyo Doa

A. 2 Petro 3:10-11 Watu wa tabia gani.
B. 2 Petro 3:14 Bila mawaa au aibu.

Tamati

*Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. —1 Yohana 1:9*



# MAVAZI YA HAKI

Bwana-arusi aliingia chumbani na kumtazama bibi-arusi wake, ambaye alikuwa ameng'ara kabisa; na ambaye alikuwa amesubiri kwa hamu na ghamu ili aweze kuunganishwa milele na kipenzi chake cha maisha. Huku akiwa amevaa nguo nyeupe kama theluji, vazi ndefu hadi miguuni, vazi ambalo halikuwa na doa, uso wake ulikuwa unametameta alipokuwa akimkaribisha bwana-arusi wake kwa furaha kuu. Muda uliokuwa umesubiriwa kwa kipindi kirefu hatimaye ulikuwa umewadia.

"Haki ya watakatifu ni jambo ambalo linawezeshwa na kazi ya damu yake Yesu, ambaye hutulipia makosa, na pia kazi ya utakaso inayotokana na athari bora zinazoletwa na Roho Mtakatifu ndani yetu."

## Bibi-arusi wa Kristo

Yohana alikuwa na maono kama hayo ya Kanisa la Mungu, ambalo lilionyeshwa kwa mfano wa bibi-arusi ambaye alikuwa ameandaliwa ili kukutana na bwana-arusi wake: "Nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe" (Ufunuo 21:2). Maono haya yanaonyesha watu wale waliokombolewa wakiwa kama mji mrembo wa Yerusalemu, na pia kama bibi-arusi: "Njoo huku, nami nitakuonyesha yule bibi-arusi, mke wa Mwana-Kondoo" (mstari wa 9). Kama bibi-arusi ambaye alikuwa amevaa vizuri ili kumpendeza bwana wake, kanisa la kweli hufanya bidii ili kumpendeza Kristo peke yake. Yesu alilipenda Kanisa, bibi-arusi wake, hivi kwamba akayatoa maisha yake "Makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa" (Waefeso 5:26-27). Mtume Paulo naye ananena kuhusu bibi-arusi wa Kristo kama "bikira safi" ambaye alikuwa ameahidiwa kwa bwana mmoja, yaani Kristo (2 Wakorintho 11:2).

Hebu basi Bwana afungue macho ya vipofu ili waweze kuona urembo wa kweli wa Kanisa moja la Mungu. Kama bibi-arusi bikira, Kanisa linastahili kujitoa nadhiri kwa Kristo peke yake, na kuweka macho yake kwake Yeye pekee. Shauku la Kanisa linastahili kuwa ni kuishi na kutenda kwa njia ambayo inamstahili Mwana wake Mungu.

## Harusi ya Mwana Kondoo

Upatanisho wa mwisho wa Kristo na Kanisa hapo mwisho wa dahari huonyeshwa kama harusi. Ufunuo 19:7-8 ina taswira hiyo ya urembo wa bibi-harusi: "Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari. Naye amepewa kuvikwa kitani nzuri, ing'arayo, safi; kwa maana kitani nzuri hiyo ni matendo ya haki ya watakatifu." Bibi-arusi, ambaye amejiandaa vilivyo na amevalishwa mavazi safi meupe, mavazi ambayo yanawakilisha haki—yaani usafi, matendo mema, maadili bora, na mambo yote ambayo ni ya kweli na haki. Haki ni swala la hali ya ndani ya mwanadamu, pamoja na tabia ambazo zimefanywa na kukubalika mbele zake Mungu. Haki ya watakatifu ni jambo ambalo linawezeshwa na kazi ya damu yake Yesu, ambaye hutulipia makosa, na pia kazi ya utakaso inayotokana na athari bora zinazoletwa na Roho Mtakatifu ndani yetu.

Watu wengi wanaokiri kuwa ni Wakristo wamepaka uchafu mavazi yao kutokana na dhambi, na wanaishi kwa njia za kidunia, lakini watu wa kweli wa Mungu hujiandaa kukutana na Bwana-arusi kwa njia ya kuishi kwa usafi na utauwa. Wale ambao watashinda dhambi "watavalishwa mavazi meupe" (Ufunuo 3:4-5), ambayo ni ishara ya usafi na kutokuwa na dosari maishani. Ni wale tu ambao watadumisha mavazi yao humu duniani yakiwa safi ndio wataingia katika utukufu, kwa maana watu wasafi ndio tu wataingia Mbinguni (Ufunuo 7:9).

## Usafi wa Moyo


Yesu alikuja na kutoa maisha yake ili watu wake wamtumikie kwa "utakatifu na haki" (Luka 1:75). Haki ya kweli sio tu ya mambo yanayoonekana, bali ni usafi wa ndani wa moyo wa mtu. Watu wa Mungu wanastahili kuishi kwa njia ya haki. 1 Yohana 3:6-8 inafundisha kwa njia ya wazi kwamba wale ambao wanadumu ndani yake Kristo hawaishi

*(Endelea katika Ukurasa 6)*

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)*
katika dhambi, kwa maana Kristo alikuja "kuangamiza kazi za ibilisi." Waumini wameitwa ili kuishi kama vile Kristo alivyoishi—kwa haki. "Na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki . . . vivyo hivyo sasa vitoeni viungo vyenu vitumiwe na haki mpate kutakaswa" (Warumi 6:18-19).

## Wito wa Haki

Maandiko wakati mwingi yanafanya wito kwa watu kutafuta haki badala ya kufuatilia tamaa za ulimwengu ambazo ni za mpito, au tamaa za kimwili. Yesu alitwambia "Utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake" (Mathayo 6:33). Wakristo wamehimizwa kutoroka dhambi na badala yake "ukafuate haki, utauwa, imani, upendo . . ." (1 Timotheo 6:11). Watu wengi hujidai kwamba wanamfuata Kristo huku wakiwa wangali wanaishi dhambini na katika hali ya udhalimu. Lakini Mtume Paulo anafanya wito kwa Kanisa katika Efeso 4:24-25 "Mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli." Haki huja kwa mtu kwa njia ya kazi ya kiungu ya Mungu pekee, na mtu huishi kwa haki hiyo kupitia maamuzi na machaguo yake ya kila siku.



"Haki ya watakatifu ni jambo ambalo linawezeshwa na kazi ya damu yake Yesu, ambaye hutulipia makosa, na pia kazi ya utakaso inayotokana na athari bora zinazoletwa na Roho Mtakatifu ndani yetu."

Ujumbe wa Mtume Paulo kwa Kanisa ungali unafaa kwa ajili yetu leo: "Amkeni ili mtende mema" (1 Wakorintho 15:34). Watu wengi wamelala kiroho, na wameruhusu mavazi yao yawekwe uchafu na mambo ya kidunia. Wakristo wanahitaji utambuzi ili waweze kujua ni matendo gani ni ya haki, na ni yapi ni ya udhalimu. Maandiko yalitolewa ili "kutufundisha kwa ajili ya haki" (2 Timotheo 3:16), lakini watu wengi wanapuuza neno lake Mungu, na kujitoa kwa athari za kizazi hiki kiovu. Lakini ukweli huweka wazi hadaa za adui yetu, na maamuzi yanayofaa yanastali kuwa ndio kanuni na haki kuwa timazi (Isaya 28:17) ya kupima mambo yote.

## Bibi-arusi na Kahaba

Maono ya Yohana katika Ufunuo yana malinganisho ya makanisa mawili. Katika sura ya 12 bibi-arusi wa kweli wa Kristo anaonyeshwa huku akiwa amevalishwa jua, akiangaza ukweli na usafi. Katika sura ya 17 mwanamke mwingine anaonyeshwa, huku akiwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu, na kito cha thamani. Mwanamke huyu ambaye alikuwa amefanya uzinzi wa kiroho anaitwa kahaba. Yeye anawakilisha Babiloni, mji ambao huwa ni ishara ya dini za Kikristo ambazo hata ingawa zinamkiri Kristo kama Bwana, zinadumu katika hali ya ukosefu wa haki, na kuruhusu matendo ya dhambi kuendelea. Hizo hutia dosari mafundisho ya kweli ya Biblia, ili kuwapendeza watu. Je, wewe ni mshiriki wa kanisa gani—ile ambayo ni safi na ambayo haina dosari, au ile ambayo inaonekana kuwa ya kupendeza watu kwa misingi ya maneno matamu, miradi yake, na ustadi wake wa maongezi, lakini ambayo inavumilia matendo ya dhambi na uchafu?

Isaya 1:21-22 inachora taswira ya wana wa Israeli kama ambao wakati mmoja walikuwa ni mji mwaminifu, lakini baadaye wakawa kahaba. Hata ingawa wakati mmoja haki na maamuzi bora yalidumu ndani ya kuta zao, wao walianza kujichanganya na ibada ya sanamu na mafundisho yasiyo ya kweli. Wakristo wengi ambao wanakiri imani yao pia wao wako katika hali kama hii siku hizi zetu. Wao wamekuwa watu ambao hawana uaminifu kwa bwana-arusi, na kwa sasa wao hawajavalishwa vazi la haki ya Mungu.

## Ahadi kwa Wenye Haki

Kuishi tukiwa tumevalishwa mavazi ya haki ni kuishi katika hali ya ajabu na iliyobarikiwa. Kuna ahadi nyingi ambazo zimetolewa kwa kwenye haki. "Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, na masikio yake husikiliza maombi yao" (1 Petro 3:12). "Bali katika kila taifa mtu amchaye na kutenda haki hukubaliwa na yeye" (Matendo 10:35). "Lakini mjapoteswa kwa sababu ya haki mna heri" (1 Petro 3:14). "Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa" (Mathayo 5:6). Juu ya yote kuna taji la haki na uhai wa milele huko Mbinguni ambalo limeahidiwa kwa wale ambao watapigana vita vizuri na kuishi kulingana na Neno lake Mungu (2 Timotheo 4:7-8).

## Wito wa Kuishi kwa Haki

Yesu anarudi hivi karibuni kama mwizi anavyofika nyakati za usiku. Dunia hii itaangamizwa, na sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu. Tukijua hili, na tukijua kwamba Kristo anarudi kuwachukua watu walio safi na watakatifu, "Imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa" (2 Petro 3:11). Wito huu wa utakatifu unaguza kila sehemu ya maisha yetu—roho zetu, mielekeo yetu, malengo yetu, maneno, matendo, mambo tunayosikiliza au kutazama, mavazi tunayovaa, mahali tunapotembea, mahusiano yetu, na hata itikadi tunazoamini. Je, mambo haya yote yametengamana na haki maishani mwako? Je, maisha yako ni matakatifu na safi? Je, yanaangazia bibi-arusi bikira wa Kristo? Petro anaendelea katika mstari wa 14: "Fanyeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake."

Vazi lako la harusi liko katika hali gani? Je, lina mikunjo ya kilimwengu au madoa ya dhambi? Je, unavaa mavazi yanayompendeza Kristo au kujipendeza wewe mwenyewe na wale walio karibu nawe? Inawezekana mtu kuishi maisha ya haki kupitia kwa nguvu zake Kristo.

Ikiwa hujavalishwa haki yake Mungu, hebu basi nyenyekea mbele zake Mungu na kuomba ili upate kazi yake ya kiungu moyoni mwako. "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yonana 1:9). Hebu tuishi kila siku huku tukiwa tayari kukutana na Kristo, kwa sababu Yeye anakuja hivi karibuni. ■

# Maswali na Majibu

## Swali: Je, mtu huhesabiwa kuwa mwenye haki kwa kufuata mafundisho ya Kanisa lake?

Swali hili linaguza kiini na maana halisi ya mtu kuwa mwenye haki. Mtume Paulo alishughulikia swala hili mara nyingi huku akijaribu kutegua mgogoro uliokuwepo kati ya Wakristo Wayahudi na Wakristo kutoka kwa watu wa Mataifa, ambao walikuwa wameoka hivi majuzi. Wayahudi wengi walijaribu kutafuta haki kwa njia ya kufuata kwa dhati matambiko na amri zilizokuwa katika Sheria ya Musa. Vivyo hivyo, watu wengi katika Kanisa la leo huchukulia kwamba miongozo na mafundisho ya dhehebu zao ndio njia ya wao kuwa wenye haki.

> "Haki hupatikana kwa njia ya imani katika kazi ya kiungu ya Kristo, sio kwa kufuata msururu wa miongozo."

Walakini, Mtume Paulo anasema wazi kwamba haki ya kweli haiwezi kupatikana kwa njia ya matendo yetu. Wagalatia 2:16 inasema hivi: "Hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa imani ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini Kristo Yesu . . . maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki."

Kulingana na mpango wa Mungu, haki hupatikana kwa njia ya imani katika kazi ya kiungu ya Kristo, sio kwa kufuata msururu wa miongozo. Haijalishi miongozo na itikadi hizo za dini ni nzuri kiasi gani, haziwezi kamwe kumletea mtu wokovu. Kuhesabiwa haki—kutangazwa kuwa "huna makosa" au "uliyekubalika" mbele zake Mungu—hakutokani na juhudi zetu wenyewe. Badala yake sisi hufanywa wenye haki kwa njia ya imani, kwa maana haki hiyo inatokana na hali ya mtu moyoni, wala sio kwa njia ya matendo ya kuonekana.

Watu wanaweza kuomba, kutoa dhabihu, kusifu, kupeana pesa zao, kuvaa mavazi ya kiwango cha wastani, na kufanya mambo mengine mazuri, lakini matendo haya yote hayaweza kubadilisha hali yao ya moyo. Hata mtu ambaye hamwamini Mungu anaweza kufanya vitendo hivyo. Ni kwa njia ya kazi ya kiungu ya Mungu pekee ndipo mtu huweza kufanywa "kukubalika" machoni pake Mungu. Warumi 5:1 inatufundisha kwamba, "Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo." Na hapo baadaye, katika Warumi 5:18-21, Paulo anaeleza kwamba ni kupitia kwa kutii kwake Kristo ndipo watu wengi walifanywa wenye haki. Haki hii huja kwa njia ya mageuzi ya moyoni ambayo hupitia kwa nguvu za damu ya Yesu na kazi ya Roho Mtakatifu.

Hata ingawa matendo mema na utii kwa Neno la Mungu huja kwa njia ya moja kwa moja kutoka kwa moyo ambao umegeuzwa, matendo haya yenyewe hayaleti haki yake Mungu; badala yake haya ndio matunda ya haki, sio kiini chake.

Kwa upande mwingine, ni muhimu kwetu kutambua umuhimu wa matendo mema. Mtu ambaye amevalishwa haki ya Mungu atafanya bidii kumtukuza Yeye katika maisha yake ya kila siku, huku akienenda kwa utakatifu na kutaka kuendelea kukua kila wakati katika neema zake Kristo. Lakini ni lazima tuwe waangalifu ili tusitegemee matendo hayo kama kiini cha kukubalika kwetu na Mungu.

Haki haipatikani (tu) kwa mtu kufuata mafundisho ya Kanisa lake. Badala yako inapatikana kupitia kwa imani katika nguvu za Yesu ambazo huleta mageuzi, jambo ambalo huzaa matendo mema yanayotokana na moyo wa haki.

"**Matendo yetu yote ya haki** yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi" – Isaya (Isaya 64:6)

"Maana nawaambia ya kwamba, **haki yenu isipozidi** hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni" – Yesu (Mathayo 5:20).

"**Si kwa sababu ya matendo ya haki** tuliyoyatenda sisi" – Paulo (Tito 3:5).

"Vivyo hivyo ninyi nanyi, **kwa nje mwaonekana na watu kuwa wenye haki**, bali **ndani mmejaa unafiki na** maasi" – Yesu (Mathayo 23:28).

"Tena nionekane katika yeye, **nisiwe na haki yangu mwenyewe**" – Paulo (Wafilipi 3:9).

JE, WAJUA?

Utafiti umeonyesha kwamba mtu akifuata maadili bora na miongozo miema ya kiroho hili huwa ni jambo ambalo linaweza kuleta athari bora kwa afya yake ya kiakili, na pia ni jambo linaloweza kupunguza msongo wake wa mawazo, na kukuza hali bora ya afya maishani mwake. Watu ambao hushiriki katika mambo ya kidini na ya kiroho bila kukoma kufanya hivyo mara nyingi hulipoti kwamba viwango vyao vya msongo wa mawazo hupungua, na wanapata hali bora zaidi za afya. *[Maandishi ya Koenig, Harold G. Religion, Spirituality, and Health – Dini, Mambo ya Kiroho, na Afya – International Journal of Psychiatry in Medicine, 2008].*

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# KUIMBA WAKATI WA TAABU

*Lakini panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu, na wafungwa wengine walikuwa wakiwasikiliza.* —Matendo 16:25



Huku wakiwa kazini ya kimisheni wakimtumikia Mungu, Paulo na Sila walishikwa, wakavuliwa nguo, wakachapwa mijeledi, na kuwekwa korokoroni. Lakini usiku wa manane wakiwa gereza la ndani kabisa, na miguu yao ikiwa imefungwa minyororo, watu hawa waliojaa damu walianza kuimba na kumsifu Mungu kwa nyimbo.

Ndipo kukawa na tetemeko kubwa la ardhi; milango ya gereza ikafunguka, na wafungwa wakawa huru. Hata ingawa muujiza wa ajabu ulifanyika usiku huo, wandugu hawa walikuwa wakiimba katika shida zao hata *kabla* ya ukombozi wao kufika. Hebu Bwana atusaidie ili tupate mahali hapo pa siri katika uhusiano wetu naye, mahali ambapo tunaweza kuimba hata wakati tungali na shida za maisha haya.

[Maandishi yaliyopo hapa chini yametolewa kutoka kwa jalida lilioandikwa na C. W. Naylor linaloitwa *Secrets of the Singing Heart – Siri ya Moyo Wenye Wimbo*]

Maisha haya yamejaa taabu, uchungu, na hali zinazomfanya mtu kufa moyo. Ikiwa tutangojea kuwa na maisha yasiyo na matatizo ili tuwe na furaha, kamwe hatutapata furaha. Furaha ya kweli haitokani na maisha ya raha mustarehe au ukosefu wa pingamizi maishani mwetu, bali inatokana na sisi kushinda mambo haya. Mara nyingi furaha ya kweli hutoka kwa nafsi ambazo zinakumbana na changamoto nyingi za maisha.

Katika 2 Wakorintho 7:4 Paulo anaandika na kusema, "Nimejaa faraja, katika dhiki yetu yote nimejaa furaha ya kupita kiasi." Mwanazaburi pia alitambua hayo aliposema, "Na nishangilie, nizifurahie fadhili zako, kwa kuwa umeyaona mateso yangu. Umeijua nafsi yangu taabuni" (Zaburi 31:7). Kujua kwamba Mungu yuko nasi wakati wa shida ni jambo linalotuletea amani.

Yesu anajua mambo yote mazito yanayotukumba—kila jambo linalotuletea uchungu wa moyo na magumu. Hebu basi tuweke tumaini kwa neema yake, na punde si punde miyo yetu itakuwa na wimbo, kwa maana mawingu yatatuondokea.

Taabu za maisha hutufundisha wimbo wa aina tofauti, wimbo ambao unahitaji ujasiri na imani. Hizi ni nyimbo za kuwa na uhakika na Mungu, kumwamini, na kuwa na tumaini kwa ajili ya ushindi ujao. Ni nyimbo za shukrani kwa ajili ya rehema za hapo mbeleni za Mungu. Na hata ingawa ni vigumu kwetu kujifunza nyimbo hizi, hizi ni myimbo ambazo zinaweza kutuletea furaha kuu zaidi kuliko zile zinazoimbwa katika nyakati za fanaka. Hii ni kwa sababu zinatokana na imani iliyo na kina kikubwa. Basi haijalishi tutakumbana na majaribu kiasi gani, ikiwa tutamtumaini Mungu tungali tunaweza kuimba wimbo wa nyakati za taabu. ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA